



**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
(VETA)**



TAARIFA KWA UMMA

**MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA ELIMU NA MAFUNZO YA
UFUNDI STADI KWA MSIMU WA MWEZI DESEMBA, 2025**

1 UTANGULIZI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) iliendesha Mitihani ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Msimu wa Mwezi Desemba, 2025 ikiwa ni hatua za kutathmini umahiri uliopatikana katika kipindi husika cha mafunzo katika ngazi ya 1, 2 na 3. Mitihani hiyo ilihusisha jumla ya watahiniwa 40,973 waliofanya mitihani katika programu zifuatazo: Programu ya Kupima Umahiri (CBA), Programu maalum ya Uanagenzi Pacha (DATS), Programu ya Mafunzo ya Biashara (NABE) na Programu ya Uanagenzi Katika Fani za Madini (IMTT). Wastani wa ufaulu kwa programu zote nne (4) ni asilimia 81.1.

2 MATOKEO

VETA inawatangazia wahitimu na wananchi kwa ujumla kuwa matokeo ya mitihani hiyo yako tayari. Matokeo yanapatikana kwenye vyo vyote vya VETA nchi nzima au kupitia tovuti ya VETA ambayo ni www.veta.go.tz au kupitia kiunganishi <https://www.veta.go.tz/december2025results>

3 MCHANGANUO WA MATOKEO

**3.1 MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
STADI KATIKA MFUMO WA CBA**

Mchanganuo wa ufaulu kwa kila ngazi ni kama ifuatavyo:

I. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Kwanza (Level 1)

Jumla ya watahiniwa 15,805 walifanya mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA katika ngazi ya kwanza ambapo watahiniwa 13,463 sawa na

asilimia 85.2 walifaulu mitihani hiyo. kati yao, wakiume walikuwa 8,784 (85.2%) na wa kike ni 4,679 (85.2%).

II. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Pili (Level 2)

Jumla ya watahiniwa 21,746 walifanya mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA katika ngazi ya pili ambapo watahiniwa 17,045 (78.4%) walifaulu mitihani kati yao, wakiume walikuwa 11,724 (82.5%) na wakike ni 5,321 (70.7%).

III. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Tatu (Level 3)

Jumla ya watahiniwa 2,700 walifanya Mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA katika Ngazi ya Tatu ambapo jumla ya watahiniwa 2,216 sawa na asilimia 82.1 walifaulu, kati yao wakiume ni 925 (80.9%) na wakike ni 1,291 (83.0%).

IV. Watahiniwa wanaopaswa kurudia mitihani kwa ngazi zote

Watahiniwa 7,527 (18.7%) kati ya 40,251 waliofanya Mitihani ya CBA kwa Ngazi ya 1, 2 na ya 3 wanapaswa kurudia Mitihani hiyo.

3.2 MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA PRAGRAMU YA TAIFA YA ELIMU YA BIASHARA (NABE)

Jumla ya watahiniwa 161 walifanya Mitihani ya Taifa ya Elimu ya Biashara katika hatua ya 1, 2 na 3, ambapo jumla ya watahiniwa 26 (16.1%) walifaulu mitihani na watahiniwa 135 (83.9 %) wanapaswa kurudia Mitihani hiyo.

3.3 PROGRAMU YA UANAGENZI PACHA (DATS)

Jumla ya watahiniwa 507 walifanya mitihani ya Programu ya Uanagezi Pacha ambapo 454 sawa na asilimia 89.5 walifaulu, kati yao wakiume 300 sawa na asilimia 87.5 na wakike 154 sawa na asilimia 93.9

.

3.4 PROGRAMU YA UANAGENZI KWENYE FANI ZA MADINI (IMTT)

Jumla ya watahiniwa 54 walifanya mitihani ya Programu ya Uanagenzi kwenye Fani za Madini (IMTT), ambapo watahiniwa 33 sawa na asilimia 61.1 walifaulu mitihani, kati yao wakiume 31 sawa na asilimia 59.6 na wakike 2 sawa na asilimia 100.

3.5 WATAHINIWA WALIOFUTIWA MATOKEO

Watahiniwa 40 sawa na asilimia 0.1 walijihusisha na vitendo vya udanganyifu wakati wa Mitihani ya Msimu wa mwezi Desemba 2025. Watahiniwa hao wamefutiwa matokeo yao yote kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya Utahini na Utunuku.

IMETOLEWA NA

**MKURUGENZI MKUU, VETA
TAREHE 02 APRILI 2026**